**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

# ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIA NCHI KATIKA MIFUMO YA HALI YA HEWA NA MWENENDO WA MVUA ZA MASIKA, 2022.

**Dar es Salaam, 13 Aprili, 2022:**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo uliohuishwa wa msimu wa mvua katika kipindi cha Machi – Mei, 2022, ushauri kwa wadau wa sekta mbalimbali kama vile Kilimo na Usalama wa Chakula, Mifugo na Wanyamapori, Maliasili na Utalii, Nishati na Maji, Mamlaka za Miji, Afya pamoja na Menejimenti za Maafa.

Kumekuwepo na vipindi virefu vya ukavu vilivyojitokeza katika kipindi cha mwezi Machi, 2022 hususan kwa maeneo ya pwani ya Kaskazini na nyanda za juu Kaskazini mashariki ambapo maeneo hayo yalipata mvua chache. Hali hiyo ya vipindi virefu vya ukavu imesababishwa na matukio ya vimbunga katika Bahari ya Hindi eneo la Rasi ya Msumbiji kusini zaidi mwa eneo ambalo lingesababisha vimbunga hivyo kuongeza mvua katika maeneo ya nchi yetu. Vile vile, yamejitokeza mabadiliko ya muda mfupi ya joto la bahari katika eneo la pwani ya Afrika Mashariki na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Mabadiliko hayo ya muda mfupi ya joto la bahari ambayo ni nadra kutokea kutokana na tabia ya bahari kutunza joto au baridi kwa muda mrefu yamesabishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mwenendo huo wa vimbunga na mabadiliko katika joto la bahari vimechangia Ukandamvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika maeneo ya kusini mwa nchi ambapo kwa kawaida katika kipindi cha mwanzoni mwa mwezi Machi huanza kuelekea maeneo ya kaskazini mwa nchi. Hali hiyo imesababisha kuvurugika kwa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kuathiri mwenendo wa unyeshaji wa mvua za Masika, 2022.

Ubungo Plaza; 388 Barabara ya Morogoro: S.L.P 3056,16102 Dar Es Salaam;
Simu: +255 22 2460706-8: Nukushi: +255 22 2460735
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Matarajio**

Katika kipindi kilichosalia cha msimu wa Masika 2022, mifumo ya hali ya hewa inaashiria kuongezeka kwa joto la bahari Mashariki mwa bahari ya Hindi sambamba na kupungua kwa joto la bahari Magharibi mwa bahari ya Hindi katika pwani ya Afrika Mashariki na hivyo kupunguza upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea katika maeneo ya nchi. Hali hii inatarajiwa kusababisha mvua za Masika, 2022 kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo ya Pwani ya Kaskazini, nyanda za juu Kaskazini mashariki na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mara, Simiyu na Shinyanga. Aidha, mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa kuendelea katika maeneo ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza pamoja na maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (Wilaya za Kibondo na Kakonko). Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani katika msimu huu wa mvua za Masika 2022, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza.

Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, 2022 katika maeneo ya pwani ya kaskazini, na kuisha kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Mei, 2022 katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini Mashariki. Aidha maeneo ya Ukanda wa ziwa Victoria mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2022.

**Athari zinazotarajiwa**

i. *Upungufu mkubwa wa unyevunyevu katika udongo ambapo hali hii inaweza kuathiri ukuaji wa mazao, upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori, upungufu wa kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini.*

ii. *Upo uwezekano wa kuongezeka kwa athari za magonjwa ya kuambukiza, hususan magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo salama kwa afya.*

iii. *Vipindi virefu vya ukavu, milipuko ya wadudu-dhurifu kwa mazao kunaweza kusababisha athari za kunyauka kwa mimea.*


iv. *Shughuli za ujenzi, usafiri na usafirishaji zinatarajiwa kunufaika katika vipindi vya mvua chache.*

**Ushauri**

i. *Wakulima wanashauriwa kuzingatia matumizi ya mbinu na teknolojia za kilimo himilivu za kuhifadhi maji na unyevunyevu wa udongo pamoja na kuzingatia maelekezo ya maafisa ugani katika maeneo yao.*

ii. *Jamii inashauriwa kuweka mpango mzuri wa matumizi endelevu ya rasilimali za maji na uhifadhi wa malisho.*

iii. *Mamlaka husika zinashauriwa kushirikiana na kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula, malisho ya mifugo, maji na kutoa miongozo ya namna ya kukabiliana na hali ya upungufu wa mvua unaotarajiwa kujitokeza.*




*Ramani: Mwelekeo wa mvua katika msimu wa Masika, 2022*

**Mvua za Msimu (Novemba, 2021-Aprili, 2022)**

Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, mvua zinatarajiwa kuendelea kupungua kadiri msimu unavyoelekea mwishoni katika mwezi huu wa Aprili, 2022. Aidha, msimu wa mvua katika maeneo hayo zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2022 kama ilivyotabiriwa awali.

*Wananchi wanashauriwa kuendelea kuzingatia taarifa na tahadhari za hali ya hewa zilizotolewa na zitakazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania sambamba na kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalam katika sekta husika ili kupunguza athari zinazotokana na hali mbaya ya hewa.*

**Imetolewa na:**
**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

Ubungo Plaza; 388 Barabara ya Morogoro: S.L.P 3056,16102 Dar Es Salaam;
Simu: +255 22 2460706-8: Nukushi: +255 22 2460735
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz